

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIFI**



Unapojobu taja: kUMB NaRDC/L.10/5VOL.III/46

Tarehe 12/07/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kutuma maombi kwa nafasi ya kazi iliyoinishwa hapa chini.

MTENDAJI WA KIJIJI III – NAFASI (2)

SIFA ZA MWOMBAJI

- Mwombaji awe amefaulu kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyefuzu mafunzo ya Astashahada Cheti **"NTA Level 5"** katika fani zifuatazo: Utawala , Sheria , Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii, Sayansi ya Jamii kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI:-

- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na usalama wa raia na mali zao
- Kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika kijiji kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya Maendeleao ya kijiji
- Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia /Sera, Sheria na taratibu katika kijiji
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika kijiji
- Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalam katika kijiji
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na mogogoro ya wananchi
- Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za kijiji

MSAHARA:-


- Cheo cha Mtendaji wa kijiji daraja la III kina mshahara wa **TGS B** kwa mwezi

MASHARTI YA JUMLA

- i. Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usipungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii. Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- iii. Mwombaji aambatanishe picha mbili za rangi za hivi karibuni (pass port size)
- iv. Mwombaji ambaye ni mtumishi wa Umma apitishe barua yake ya maombi kwa mwajiri wake
- v. Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na namba zao za simu
- vi. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali
- vii. "Testimonials " "Provisional" RESULT"result", Statement of Results" N.K hazitakubalika
- viii. Waombaji wote ambao wamesoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na **TCU** na **NECTA**
- ix. Waombaji waambatanishe nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) au waandike namba ya kitambulisho kwenye barua ya maombi.
- x. Mwisho wa kupokea barua ya maombi ni tarehe **25/07/2021** saa **9:30 Alasili.**
- xi. Barua zote zitumwe kwa anuani

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIFI
S.L.P 28
RUFIFI**

N:B Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya www.rufijidc.go.tz.



Rashid S. Salum

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji